

Nyama ya nguruwe ni salama kabisa

Na Danson Kaijage, Dodoma

SERIKALI imewatoa hofu watumiaji wa nyama ya nguruwe maarufu kama (Kitimoto) kuwa nyama hiyo ni salama kama zilivyo nyama zingine.

Hayo yameelezwa na Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania ((TVLA)), Dk Stella Bitanyi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika ukumbi wa Idara ya Habari Maelezo juu ya utekelezaji wa shughuli za wakala katika mwaka wa fedha 2022/23.

Alitoa kauli hiyo kutokana na kuwepo kwa kauli mkanganyiko kwamba nguruwe si salama kuliwa na binadamu kwa madai kwamba ana wadudu wengi wanaosababisha maradhi.

Akitoa ufanuzi Dk Bitanyi alisema nyama ya nguruwe ni salama kama zilivyo nyama zingine isipokuwa mlaji anapaswa kuhakikisha mnyama huyo amepatiwa chanjo na dawa kama inavyotakiwa.

"Nyama ya nguruwe ni salama kabisa kama zilivyo nyama zingine, unachotakiwa kuhakikisha ni kwamba unakula

nyama ya nguruwe aliyepeata chanjo zinazotakiwa, tatizo la nguruwe ana minyoo ambayo ni hatari endapo utaila kama hajauawa na chanjo, madhara yake minyoo hiyo ikiingia kwenye ubongo la mlaji, anaweza kupata matatizo," alisema Dk. Bitanyi.

Wakati huohuo wakala huo umeeleza kuwa kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2018 hadi sasa, serikali imewekeza sh 5,667,000,000 katika taasisi ya chanjo.

Dk Bitanyi alisema taasisi ya COSTECH, imefadhili miradi

miwili yenye thamani ya sh 800,000,000 inayolenga kuboresha miundombinu ya maabara ya uthibiti ubora ili kuhakikisha chanjo zinazozalishwa zinakidhi kanuni za uzalishaji bora wa chanjo (GMP) na kuzifanya zikubalike kitaifa na kimataifa.

Katika hatua nyingine Dk Bitanyi alisema kuna umuhimu wa kupima na kujuu ugonjwa unaomsumbua mnyama ili kuweza kutoa tiba sahihi.

"Matumizi holela ya dawa, hasa dawa za aina ya antibaiotiki huweza pia kuathiri binadamu

kutokana na kula mabaki ya dawa hizo kwenye vyakula vinavyotokana na wanyama.

"Hili ni tatizo kubwa linaloikabiri dunia kwa sasa na waifugaji wanapaswa kuzingatia ushauri unaotolewa ili kudhibiti," ameleeza.

Dk. Bitanyi alisema inakadirwa kuwa ifikapo mwaka 2030, watu zaidi ya milioni 10 watakuwa kutokana na dawa kushindwa kuwatibu kwani vimelea vya magonjwa vitakuwa vimejenga usugu unaotokana na matumizi holela ya dawa kwa binadamu na mifugo.

TAIFA



Wachuuzi wa samaki wakisubiri wateja katika eneo la Ukonga Banana, jijini Dar es Salaam jana. Samaki mmoja anauzwa kwa bei ya 5,000/- hadi 30,000/- kulingana na ukubwa wake. **PICHA: JUMANNE JUMA**

Kasi ya ukuaji NMB yawakosha wateja,